JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

Nukushi: 025 - 2530233
Simu Na: 025–2530404
Baruapepe:td@tundumatc.go.tz
Tovuti;www.tundumatc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji
S.L.P 73
TUNDUMA

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA UFUNDI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE YA MSINGI MLIMANI HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

02/05/2023

Shule ya Msingi Mlimani inatarajia kufanya ujenzi wa Vyumba vya madarasa, matundu ya Vyoo vya wanafunzi ikijumuisha mashimo yake, iliyoko kata ya Uwanjani katika Hamashauri ya Mji Tunduma kwa kutumia uratatibu wa 'FORCE ACCOUNT'.

Jedwali: Majengo yanayotarajiwa kujengwa katika shule husika:

| S/N | JINA LA SHULE | KATA ULIPO MRADI | AINA YA MAJENGO NA IDADI | IDADI YA MAJENGO (BLOCK) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MLIMANI | UWANJANI | Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na Ofisi 1 ya walimu | 2 |
| | | | Ujenzi wa Matundu 3 ya vyoo | 1 |

Ili kufanya kazi hiyo Kamati ya Shule inatangaza nafasi za mafundi wenye sifa za kuomba kwa kuzingatia masharti na sifa zifuatazo:

Mwombaji/Fundi Mkuu lazima awe Mhandisi Ujenzi au kiwango kinachoendana/kuhusiana na hiyo (Civil and or related Civil Engineering)/Fundi Sanifu Ujenzi (Diploma/FTC)/Fundi aliyehitimu mafunzo ya ufundi Stadi/ Msanifumajeng(Architect)/MkadirAuMkadarasimwenye Mtaalamu mwenye sifa zilizoainishwa hapo juu na kuambatanisha nakala za vyeti.

wombaji/Fundi Mkuu/mzabuni atakayeweka/kuajiri msimamizi, msimamizi huyo anatakiwa kuwa na sifa kama hizo hapo juu pamoja na uzoefu wa kazi za ujenzi wa majengo ya serikali na kutakiwa kuorodhesha miradi aliyokwisha tekeleza ikiambatana na mahali ilipo, jina, namba za simu za wamiliki wa miradi hiyo.

1. Mwombaji/Fundi Mkuu anatakiwa kuthibitisha kuwa anazo nyenzo/zana muhimu za kufanyia kazi ili kuthibitisha hili atatakiwa kuorodhesha nyenzo/zana hizo
2. Kwa uharaka wa mradi huu, Mwombaji/Fundi Mkuu anatakiwa kuwa na mafundi wasaidizi wa kutosha wenye uzoefu wa kila fani (Uashi, rangi, umeme, uselemala, nk) na kuwepo wakati wote wa utekelezaji wa mradi na kutakiwa kuorodhesha idadi yao.
3. Kwa uharaka wa mradi huu, Mwombaji/Fundi Mkuu/mzabuni hatakiwi kufanya maombi ya zaidi ya jengo moja (Block).
4. Mwombaji/Fundi Mkuu anatakiwa kutembelea eneo la mradi na kukagua, kusoma michoro kwa kazi zilizoainishwa katika fomu ya nukuu ya kazi za ufundi kabla ya kujaza gharama za ujenzi.
5. Mwombaji/Fundi Mkuu anatakiwa kujaza/kuweka gharama za ufundi katika fomu hiyo, fomu itakayowasilishwa baadhi ya maeneo hayajawekewa bei haitashughulikiwa.
6. Mwombaji/Fundi Mkuu anatakiwa awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea, mwenye makazi yanayoeleweka na barua ya maombi yapitishwe kwa Mtendaji wake wa Kata/Mwenyekiti Mtaa.
7. Mradi huu unatakiwa kukamilika kabla ya tarehe 15/06/2023, hakuna muda wa nyongeza utakao tolewa
8. Hakutakuwa na malipo ya awali kwa fundi Mkuu/Mkandarasi/Mzabuni na kwa kuzingatia umuhimu na uharaka wa mradi huu, Fundi Mkuu/Mkandarasi Mjenzi/Mzabuni lazima awe na mtaji wa Kutosha kuwalipa mafundi wazaidizi na vibarua.
9. Aambatanishe nakala ya maelezo ya kifedha (Bank statement) ya miezi angalau 3 kabla ya tarehe ya tangazo ili kuthibitisha mataji alionao wa kuwalipa mafundi wasaidizi na vibarua
10. Awe tayari kukakuguliwa na kupokea maelekezo yatakayotolewa na Wataalamu wa Ujenzi na viongozi wa Serikali watakao tembelea mradi
11. Fundi mkuu lazima aandae na kuwasilisha mpango kazi ukielezea shughuli na muda wa utekelezaji wa mradi husika.
12. Awe tayari kufanya kazi masaa 24 na kukamilisha mradi kwa mujibu wa masharti ya mkataba na kukabidhi jengo lenye kiwango kinachokubalika na kutakiwa.
13. Mwombaji/Fundi Mkuu/mzabuniatakayeweka/kuajiri msimamizi, lazima wawe na uwezo wa kusoma na kutafasiri mchoro, kufanya makadirio ya awali na mafundi wasaidizi lazima awe na uwezo wa kujenga tofali aina zote, Usukaji wa umeme (Awe aliyesajiliwa na EWURA), uwekaji mifumo ya maji safi na taka, uwekaji wa sakafu aina zote, kupaua aina mbalimbali katika majengo ya Serikali.
14. Awe mwaminifu kutumia vifaa anavyokabidhiwa
15. Fundi Mkuu/Mzabuni/Mkandarasi lazima awasilishe bahasha moja yenye bahasha mbili tofauti (Moja iwe na viambatanishi vya mahitaji ya tangazo hili ambapo bahasha nyingine iwe na nukuu za gharama za ufundi zilizojazwa vizuri kwa ukamilifu)

16. Awe na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN Number)

17. Awe na akaunti ya bank iliyo hai

18. Maombi yote yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili na kufungwa vizuri na kuandikwa juu ya bahasha kwa herufi kubwa :nb kablasha la zabuni linapatikana kwa mkuu wa shule

    **MWENYEKITI WA KAMATI YA UJENZI**

    **SHULE YA MSINGI MLIMANI**

    **S.L.P73TUNDUMA**

19. Mwisho wa kupokea maombi ni Tarehe 10/5/2023, saa 04:00 asubuhi siku ya Jumamosi na ndiyo siku ya ufunguzi, maombi yote yatafunguliwa hadharani. Hivyo Mwombaji/Fundi Mkuu/Wazabuni/Wakandarasi au wawakilishi wa waombaji wanaombwa kuhudhuria wawakilishi wao wanaombwa kuhudhuria siku ya ufunguzi.

20. Maombi ambayo yatafika baada ya muda tajwa hapo juu hayatapokelewa hata kwa sababu yoyote ile

**TANGAZO HILI LIMEANDALIWA NA**

..........................................................

EDSON MWASALEMBA

**MKUU WA SHULE**

**HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA**

**Namba ya mkuu wa shule 0764000500**

**Mwenyekiti 0783939498**